

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



11 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 11 JUNI, 2015

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2015/2016.

WAZIRI WA FEDHA:

Taarifa ya Sera za fedha kwa kipindi cha Mwaka 2014/2015 na Mwelekeo wa Sera za fedha kwa Mwaka 2015/2016.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

185. MHESHIMIWA SYLVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mifuko ya elimu iliyoanzishwa katika Majimbo, Halmashauri na Wilaya kwa lengo la kuboresha ubora wa elimu.

186. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Wilaya ya Mlele imepeleka maombi ya kupandishwa hadhi Kituo cha Afya Inyonga kuwa hospitali ya Wilaya lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika:-

Je, kuna kikwazo gani katika kutekeleza jambo hilo.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

187. MHESHIMIWA SALUM KHALFAN

BARWANY (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kuna taarifa kupitia vyombo vya habari kuhusu juhudi za Serikali kutoa taaluma ya Gesi na Mafuta:-

- (a) Je, Wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara wananufaikaje;
- (b) Je, ni vijana wangapi hadi sasa wamepatiwa mafunzo na wapi.

188. MHESHIMIWA DAVID ZACHARIA KAFULILA (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Tarafa ya Nguruka katika Wilaya ya Uvinza ni tarafa yenye watu wengi, uchumi mkubwa na tarafa ya kwanza yenye huduma ya benki lakini haina umeme:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika tarafa hiyo.

WIZARA YA UJENZI:

189. MHESHIMIWA AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wamiliki wa winchi za kuondoa magari yaliyopata ajali barabarani na Askari wa Usalama Barabarani kwa kutolipa pesa za wamiliki hao:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatunga sheria itakayowawajibisha wamiliki wa magari yaliyopata ajali kulipa gharama ya kunyanyua magari yao badala ya kuwatumia Askari wa Usalama Barabarani kuwakusanyia pesa wamiliki wa magari hayo;
- (b) Je, kuna bei elekezi inayotumika kuwaongoza wamiliki wa winchi kwa kazi ya unyanyuaji wa magari yaliyopata ajali;
- (c) Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa wamiliki wa magari yaliyopata ajali pale wanapochelewa kuita winchi ya kuondoa magari barabarani.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

SAA 10.00 JIONI:

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

**DODOMA
11 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**